



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD**

Wednesday, 6th March, 2024
Third Assembly – Third Session
ELEVENTH SITTING

*[The County Assembly met at 10:10a.m. at the County Assembly Buildings]
[The Speaker (Honourable Aharub Ebrahim Khatri) in the Chair]*

PRAYERS

The Speaker (Hon. Khatri): Good morning. Honourable Members, you may be seated. Yes Clerk? Next order please?

PAPER

WARD OFFICE MANAGEMENT POLICY

Yes, Honourable Athman Mwamwiri, Leader of Majority Party? Please lay the Paper.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker, I wish to lay paper Ward Office Management Policy, 2023.

[Paper laid]

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Members, the Paper stands committed to Committee on Justice and Legal Affairs for consideration. Yes, Clerk? Next order please?

MOTION

MEASURES TO ADDRESS SHORTAGE OF FRESH WATER IN MOMBASA COUNTY

Yes, Honourable Maryam Baimu MCA Free Town please move the Motion.

Hon. Baimu: Thank you so much Mr. Speaker. Mr. Speaker, I beg to move the following Motion;

AWARE THAT, water is a fundamental human right recognized by international treaties and enshrined in Article 43(1) (d) of the Constitution of Kenya;

FURTHER AWARE THAT, the Fourth Schedule of the Constitution assigns the County government the mandate to address water and sanitation and acknowledging the Water Act (2016) and other relevant legislation;

NOTHING THAT, access to clean and sufficient water is crucial for public health, economic development, and the realization of basic human rights;

APPRECIATING the efforts of His Excellency the Governor in emphasizing the importance of water resource management;

ACKNOWLEDGING the existing shortage of fresh water in Mombasa County, affecting citizens, County buildings, and offices;

CONCERNED THAT the current situation poses a severe threat to public health, economic activities, and the overall well-being of Mombasa County residents;

DEEPLY CONCERNED THAT, despite earlier resolutions, the water shortage situation persists, exacerbating the hardships faced by the residents;

I, therefore, urge this Assembly to RESOLVE:

- 1. THAT the County government takes immediate steps to address the shortages of fresh water in Mombasa County, including County buildings and offices;*
- 2. THAT water infrastructure is upgraded and expanded to ensure a reliable and sustainable water supply;*
- 3. THAT public awareness campaigns are conducted to educate residents on water conservation and efficient water use practices;*
- 4. THAT the County government collaborates with relevant stakeholders to explore alternative water sources and technologies;*
- 5. THAT the County government allocates adequate funds to implement these measures effectively;*
- 6. THAT the relevant county departments work in coordination to streamline water management efforts;*
- 7. THAT the County government engages in partnerships with external agencies to access technical expertise and financial support for water projects.*

Honourable Katana, kindly second my Motion. Thank you.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Katana?

Hon. Katana: Thank you, Mr. Speaker Sir. I stand to second the Motion.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Members. Honourable Members, I now propose the question that the motion by Hon. Maryam Baimu on Measures to Address Shortage of Fresh Water in Mombasa County be considered by this Hon. House in the same terms as mover?

[Question proposed and agreed to]

Yes, Honourable Maryam Baimu please make your contribution.

Hon. Baimu: Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker Sir, therefore I propose resolutions urging the County government to take immediate and substantive measures to mitigate the water shortage in Mombasa County. Upgrading and expanding water infrastructure is a crucial step towards ensuring a reliable and sustainable water supply for residents. Also, it can construct large water resistance so as to assist. Public awareness campaigns on water reservation and efficient water use practices are essential, to instil a sense of responsibility among our citizens. Furthermore, Mr. Speaker collaboration with relevant stakeholders to explore alternative water sources and technologies will contribute to a more resilient water supply system and also, we can desalinate the water. Mr. Speaker Sir, allocating adequate funds to implement these measures effectively is paramount. We must prioritise the well being of our residents and overall development of Mombasa County by investing in sustainable water management solution. Mr. Speaker Sir, co-ordination among relevant County Departments is vital for the success of these initiatives; by working together we can stimulate water management effort and ensure a more efficient response to the challenges at hand. KPLC bills that most of the time do not get paid by the County government, I believe if we can get them paid in time, this problem will be assisted or will be long gone. Also Mr. Speaker Sir, in engaging in partnership with external agencies to assist technical expertise and financial support for water projects will enhance our capability and broaden the scoop of potential solution. Together we can address the water shortages in Mombasa County, comprehensively and improve the quality of life for all our citizens. Mr. Speaker Sir, I therefore call upon all Members of this Assembly, to support these resolutions for the greater good of Mombasa County and its residents thank you Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Maryam Baimu for your contribution. Yes, Honourable Allen Katana please make your contribution.

Hon. Katana: Mheshimiwa Spika nikushukuru kwa nafasi hii na mimi nitoe mawazo yangu kuhusiana na suala hili Mheshimiwa Spika, kama tunavyojua wanasema maji ni uhai na hasa kwetu Mombasa kama maji kweli ni uhai basi uhai wa watu wa Mombasa Mheshimiwa Spika uko hatarini sana kwa sababu ya ukosefu wa maji mara kwa mara Mheshimiwa Spika. Kama vile Mheshimiwa Maryam Baimu aliyetoa hoja hii kwamba ametoa ombi ya kwamba Serikali yetu ya Kaunti ikaweze kutengeneza mabirika makubwa ili wakati itakapokuwa maji yapo yakaweze kujaa kwa mabirika ili tusiweze kukosa maji mara kwa mara hata Kaunti jirani hapa. Nakumbuka Mheshimiwa Rais wa sasa wakati akiwa Naibu wa Rais alikuja akafungua mabirika makubwa sana ambayo yanasaidia kuhifadhi maji Mheshimiwa Spika na ikapunguza kwa kiasi fulani matatizo ya maji pale Kilifi Kaunti. Vile vile imekuwa ni ombi ikiwa Mombasa tutakuwa na mawazo kama hayo tena Mheshimiwa Spika nitoe ombi kupitia kwa suala hili ya kwamba Kamati yetu nzuri inayofanya kazi kwa bidii inayoshughulikia masuala ya maji ipewe nafasi kupitia kwa heshima yako wakaweze kutembelea Baricho na huku Mwache ambako kunatoka maji haya.

Hii ni kwa ajili wakaweze kujua matatizo ni gani hasa ili tukiweza kuishauri serikali yetu ya Kaunti tuipe ushauri mwafaka utakao wasaidia watu wetu katika maji safi ya kutumia. Kwa hiyo Mheshimiwa kwa hayo machache Mheshimiwa Spika niruhusu niunge mkono Hoja hii ya maana sana. Ahsante.

[The Speaker [Honourable Aharub Ebrahim Khatri) exited the Chair]

[The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani) in the Chair]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Leader of Majority?

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono Hoja hii. Hoja hii Mheshimiwa Spika mojawapo wa zile haki za kibinadamu lakini pia kwa mujibu wa malengo ya maendeleo endelevu (SDGs) ambayo ni ruwaza ya umoja wa mataifa katika yale malengo yake 17 Mheshimiwa Spika lengo la 6 linazungumzia swala la maji na usafi Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika katika hili kwa sababu ni lengo ambalo dunia inapania kwa mujibu wa umoja wa mataifa kuweza kufikiwa inapofika Mwaka wa 2030 ipo haja sisi kama Gatuzi Mheshimiwa Spika ikiwa hii ni mojawapo ya majukumu yetu kuchukua hatua za mbele kusimama kidete kuhakikisha ya kwamba tunafikia malengo haya. Mheshimiwa Spika katika maombi ya Mheshimiwa aliyetoa Hoja hii amesema pia Serikali tuisitize masuala ya ubia ama ushirikiano Mheshimiwa Spika na pia katika malengo ya maendeleo endelevu Mheshimiwa Spika lengo la mwisho ama lengo la 17 limesisitiza ushirikiano katika kuweza ama katika kuwezesha malengo haya ya maendeleo endelevu Mheshimiwa Spika. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika Hoja hii iko sambamba na ruwaza ya kitaifa, ruwaza ya kidunia lakini zaidi katika malengo endelevu ya umoja wa mataifa hivyo basi nisisitize tu Waheshimiwa ya kwamba tuweze kuunga mkono na vile vile kuhusu kusukuma utekelezaji wake ili tusiwe katika changamoto tunazopitia sasa hivi changamoto za ukosefu wa maji na Mheshimiwa Spika pia kuna mnene mmoja alilumba akaamba ya kwamba mfa maji baharini ni mzembe Mheshimiwa Spika kwetu sisi Mheshimiwa Spika asilimia kubwa ya ardhi yetu ni bahari lakini leo tunazungumzia ukosefu wa maji na tushaambiwa mfa na kiu baharini ni mzembe. Kwa hivyo sisi Mombasa kubakia na kiu wakati bahari tunayo itakuwa ni uzembe Mheshimiwa Spika na haipendezi...

[Applause]

Katika karne hii ya sasa chini ya uongozi wetu sisi ambao Mwenyezi Mungu ametupatia hekima, elimu, busara na uwezo wa kutekeleza yanayostahiki kuitwa wazembe kwa sababu Mombasa hakuna maji na wakati imezungukwa na maji. Ahsante Mheshimiwa Spika naunga.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Ibrahim Omondi?

Hon. Omondi: Thank you. I think am audible enough...

[Honourable Omondi declined to hold the microphone]

Thank you, Mr. Speaker for giving me this humble opportunity so that I may express my views towards this admirable Motion that we are having today. I want to contribute towards this Motion that we are having today; shortage of fresh water in our County of Mombasa. We all know that water is not just a luxury but a fundamental human right that we owe every citizen in this country, if not County. As representatives of our people, we have a responsibility to confront and also sort pressing issues of our people in our County Mr. Speaker, water being one of them. Mr. Speaker, you know in Mombasa actually the residents of Mombasa are *[Inaudible]* on water on a very high level and that is part of our daily needs and the scarcity of the vital resource causes a great threat to public health, sanitation and economy's prosperity. Mr. Speaker, families are forced to endure the burden of insufficient water supply grabbing with the daily struggle to ensure even the most basic requirement for sustenance and hygiene. Our responsibilities as elected leaders or elected officials is to ensure that we take the steps to address the crisis and ensure equitable access to clean, safe and reliable water to all residents of Mombasa County. Now this Motion provides us with a timely opportunity for all of us to demonstrate our commitment and the well-being of our constituents and to uphold to the principle of justice and equality and therefore I urge all Members of this County Assembly that we all join hands to support this fundamental Motion. Thank you, Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Leila Nyache?

Hon. Nyache: Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwanza naomba msamaha kwa sababu nimechelewa kidogo hata nilikuwa naipitia kwa sababu mimi ndio Mwenyekiti wa maji Kaunti ya Mombasa nisiweze kujibu ama kuchangia mambo yasioeleweka. Lakini nimepitia kidogo naona nimesimama pia kuunga mkono hoja hii iliyokuja na Mheshimiwa mwenza dada yangu Maryam Baimu. Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kweli Mombasa kuna shida ya maji na maji masafi ilikuwa ni matatizo afadhali kuna visima kidogo viko sihaba lakini maji safi inakuwa ni shida. Kwa hivyo mwenzangu amekuja na hoja hii, mimi ningeomba sote tuweze kuiunga mkono ama tuweze kutilia mkazo haswa kwa idara ya maji tuweze kutilia mkazo waweze kushirikiana na mashirika mbalimbali tuweze kupata maji safi kwa watu wetu wa Mombasa. Ahsante Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Fatma Mote?

Hon. Fatma Swaleh: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kuweza kunipa fursa hii. Mheshimiwa Spika, nimesimama kama Mheshimiwa wa Kadzandani ambaye sikuibiwa kura na vile vile nimesimama kuunga mkono hoja ambayo imeletwa na Mheshimiwa jirani Mheshimiwa mama Mariam Baimu, Mheshimiwa ambaye alikuwa Chifu, ana akili ya kuweza kufikiria kwamba bila maji hakuna kupika, hakuna kula, hakuna kuoga, hakuna usafi Mheshimiwa Spika. Kwanza twatafikana tufahamu hilo na vile vile bila maji ungekuwa huko hapo, ungekuwa hukuchana nywele, kwa hivyo tuweze kufahamu kwamba maji ni uhai. Kama unavyojua Mheshimiwa Spika sisi Waislamu kwanza tukianza kuoga tunaanzia kichwa ili tuwe tohara; bila kujitoharisha yaani bila maji wengine huwa ni ngumu sana kujitoharisha na kuweza kuja kazini maanake ukija bila tohara huwezi kuswali na hayo ni maji. Mheshimiwa Spika huwezi kujitoharisha na mchanga ukasema unakuja kazini na udhu mpaka maji; kwa hivyo Mheshimiwa Maryam, Mheshimiwa jirani, Mheshimiwa Chifu kongole sana kwa kuweza kufikiria kuleta hoja hii.

Vile vile Mheshimiwa Spika katika kumbu kumbu zangu katika *manifesto* ya Gavana alisema shule zote za Mombasa zitakuwa na maji safi. Cha kusikitisha Mheshimiwa Spika ni mwaka umekwisha, shule yangu ya Kadzandani maji yanayonywewa ni ya chumvi! Mheshimiwa Spika ikifika wakati wa *show* sisi watu wa upande wa Nyali sote huwa tuna shida sana ya maji maana yake huwa tunaambiwa maji yanapelekwa *show*. Kwa hivyo Mheshimiwa Spika, kama vile Gavana alivyosema kwamba kutakuwa na maji safi kuanzia mashule na sisi majumbani kwetu, hata vile visima ambavyo viliweza kuwachwa na Mheshimiwa aliyekuwa wa kwanza Sultan Ali Hassan Joho aliweza kutujengea visima vingi sana hapa Mombasa, vile vile kama itawezekana Gavana aweze kuendeleza visima vile vilivyo wachwa na Mheshimiwa Gavana wa Mombasa Sultan wa Mombasa ili viweze..., wazungu wanasema kwamba *purify*, viweze kubadilishwa yaani yale maji yaweze kuwa maji *fresh*. Kwa hivyo ni hayo tu Mheshimiwa Spika naunga mkono hoja hii mia fil mia, ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you Honourable Fatma. Honourable Milka Moraa, then come to Honourable Hassan Ulkher.

Hon. Ngare: Thank you Mr. Speaker for being very considerate; you realized that I stood much earlier than Honourable Hassan. I stand in support of the Motion that has been brought by Honourable Maryam Baimu which is a very crucial Motion to the residents of Mombasa including you and I. We all know importance of water, the immediate Honourable Member has been narrating the importance of water even to our human bodies, it applies across the board, even Christians that is the same thing we do, we have to be neat, we have to be clean before we get out of our home. So, water is a very important commodity that must be in plenty in all homes, in all offices and other places and you know that lack of water causes a lot of problems. First in the priority list is the deadly disease that it causes when we do not have clean water, diarrhea, and typhoid name them, so we do not want our people to be experiencing such. I see the Chair of Water walking around and we need to take note of what is being discussed in this House so that she makes follow up in order for this crisis to be solved. Mombasa was receiving around 48 million liters of water sometimes back around 2016/2017, I remember that is when I joined this House and there was a promise that will be receiving 200million cubic litres of water through desalination.

We are hoping that is really the process that is going on and that is going to be effected so that we have as we are blessed to have the ocean, a large water mass around us, and if we do not make use of it then we shall be doing a big disservice to the people of Mombasa so desalination is what we must follow. Most of the piped water that is coming to Mombasa is from our neighboring Counties; Kilifi, Tana River and Kwale, so this is something that we must sort since we have a large water mass and desalination is the only way of sorting out this problem Chair of Water Honourable Leila Nyache should be taking this notes so that she can pick from where we are, what we are saying to deliberate with the necessary organs that are exposed to her as the Chair that mandate needs to be taken seriously so that we have people of Mombasa having clean water for the various purposes where it is supposed to serve. With that I urge Honorable colleagues to pass this Motion which is important so that we move ahead. Thank you, Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Hassan Mohamed?

Hon. Hassan Mohamed: Ahsante sana Bwana Spika kwa kunipatia fursa hii kuweza kuchangia hoja ambayo imeweza kuletwa na mamangu pale. Hii ni hoja ambayo imeweza kugusa maisha ya binaadamu, wanyama, miti na vitu vingi sana na maneno yote ambayo tumeweza kuongea ni maneno ambayo yameweza kunukuliwa katika vitabu vya dini. Nikiweza kunukuu katika Quran tukufu Mungu anasema na ndani ya maji tukajaalia kila kitu uhai na ndio maana mzungu akasema *water is life*. Maisha yetu maji ni muhimu sana hivi nilivyotoka nimetumia maji, miti inatumia maji kila kitu kinatumia maji. Wametaja vitu vingi na wamesahau kusema kuwa pia tendo la ndoa linahitaji maji, wanao chonga na wanao kula *Muguka* pia wanakunywa maji...

[Applause]

Maji ni muhimu sana Mheshimiwa Spika. Kwa hiyo kuna mambo mengi ambayo yanaweza kuja hapa katika Bunge letu yasipite lakini hili ila maji Mheshimiwa Spika nataka kulifanyia kazi maanake hata wapinzani tuliotumia maji kuwashinda maanake tuliwatia maji. Ahsante.

[Applause]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Madialo?

Hon. Madialo: Ahsante Bwana Spika. Kwa sababu hoja hii imekuwa *seconded* na Mheshimiwa Katana imesababisha niifikirie kwa undani sana ninapo jadili hoja hii na baada ya kufikiria kwa undani naiunga mkono lakini ningependa kusema hivi; kama vile Mheshimiwa Fatma Mote alivyosema ningependa kukubaliana naye kwa sababu gani na nataka Mwenyekiti wa Kamati inayoshughulika na maji wakapate kusikiza. Mwaka jana nilikuja hapa nikaleta hoja na ikapitishwa katika Bunge hili ya kwamba serikali ya Kaunti ya Mombasa ijaribu iwezavyo kuhakikisha kuwa kuna maji safi kwa shule za chekechea ambapo ni shule zao ziko kwa kiingereza *domiciled* shule za msingi na hizi shule ziko nyingi sana, ziko chini ya mia moja katika Kaunti hii. Sasa kama jambo dogo kama hilo na ukienda katika shule zetu utapata kwamba hata ukiingia kwa *gate* tayari unasikia harufu na harufu hiyo inatoka kwenye vyoo na ni hatari sana kwa watoto wadogo ambao wanasoma pale na inasababisha kwamba mtoto akiwa darasani halafu ashikwe na haja atasumbuka kisaikolojia akifikiria kwamba hivyo ndivyo vyoo wanavyoenda kuvitumia na wengi wao hawana viatu. Hivyo kuingia ndani pale katika hali na mazingira kama hayo inakuwa ni hatari sana na tumepitisha hapa mpaka sasa hivi na hili lilikuwa mwaka jana halijatekelezwa. Kama madogo hayo hayajatekelezwa haya tunaulizia jambo hili ambalo ni kubwa na lina uzito.

Kwa hivyo Mheshimiwa Spika naomba ya kwamba Mwenyekiti tunakutuma ya kwamba wakapate kujua ya kwamba jambo hili ambalo tutalipitisha hapa tunataka watu wetu wakaweze kusaidika. Ukweli wa mambo; na ninakushukuru Mheshimiwa kwa kuleta hoja hii, kuna ukosefu mkubwa sana wa maji na *transformative leadership* ni uongozi ambao *you think outside the box*. Kwa hivyo kama Mombasa kutatokezea *transformative leadership*, *let us think outside the box* vile Mheshimiwa Milka Ngare amesema kuhusu mambo ya *desalination* na tumesikia Gavana tayari ashaanza hiyo *process*. Namshukuru na ame *task* watu kuchunguza jambo hili kama itawezekana na mimi naamini ya kwamba inawezekana; Waheshimiwa mumesafiri hapa na pale na mkaona kwamba kuna nchi ambazo hazina hata mvua kwa muda mrefu na zimezingirwa na maji tu kama haya ambapo ni ya chumvi na katika hizo nchi maji yako tele maana wamefanya hayo ya kusafisha.

Hivyo basi mimi ninaamini kwamba baada ya kusafisha hawalipishi wale watu wanatumia bei gali, hivyo inawezekana na saa zengine kama Bunge lazima tuwe tuko makini sana na tutilie mkazo sana na tuhakikishe kwamba wamejua ya kwamba sisi yale ambayo tumelenga yawe ni hivyo...

[Interruption]

Mwenyekiti wa Maji sikiza...! Kama huwezi kazi jiuzulu ili tu...ngoja kidogo, *relax*! Bwana Mwenyekiti naomba unilinde...!

[Interruption]

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Proceed Honourable Madialo.

Hon. Madialo: Kwa hivyo Mwenyekiti wa Kamati ya Maji tunakupatia jukumu unaweza hata kivyako na Kamati yako na muni alike mimi kama rafiki wa Kamati twende tukaangalie huko Dubai tuone vile hayo maji wana safisha namna gani tuwe *pro active* na tulete hayo maneno tuseme kuwa kule inawezekana. Nyinyi mambo ya kusema kuwa mambo ni magumu kwa Kamati sisi tumeenda tukaona inawezekana anzeni hiyo kazi. Ahsanteni sana.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Nusura?

Hon. Nusura Mwinyi: Ahsante Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nataka nimpe pongezi sana Mheshimiwa Maryam Baimu kwa kuleta hoja hii. Kwa kweli sisi kama binadamu tunajua kuwa maji ni uzima na maji ni kila kitu kwa sababu kila sehemu inahitaji maji na inatumia maji. Lakini nataka kusema kwamba kwanza sisi kama watu wa Likoni labda tuna miaka kama 30 maji *fresh* hatuyaoni afadhali huku kwa wenzetu wengine wanapata kwa sababu sisi tunatarajia maji kutoka Marere naona huku wenzetu wanapata maji kutoka Baricho na kutoka Mzima Spring. Sasa huku kuna nafuu kidogo maji yanapatikana, sisi kule kwetu Likoni tuna shida zaidi ni miaka 30 mpaka sasa hivi hatunywi maji *fresh*, tuliahirisha mpaka matumbo yakazoea. Kwa hivyo hii hoja imekuja leo hapa Bungeni tuiunge mkono angalau na sisi kule Likoni tuwe na sahali kwa sababu Likoni pia ni Kaunti ya Mombasa lakini maji yetu twategemea Kwale. Hata huku tunategemea Kilifi na Taita Taveta lakini kwa wenzetu kuna nafuu.

Jengine ambalo nataka kulizungumzia Mheshimiwa Spika nataka kusema pengine labda pia ufisadi unachangia kama kule kwetu Likoni kwa sababu kuna wale watu ambao labda sijui nitasema ni ma bwenyenye ndio bora zaidi labda wanapata maji na wanachota maji usiku kwa sababu kuna buza ambazo zinachota maji pale *corner* mpya, labda hua zinachota usiku zikituuzia sisi kule mitaani. Nataka kusema watu wote ni bora jamani Mheshimiwa Spika wananchi wanapata shida sana kule Likoni matumbo yalizoea lakini pia kila maji yana ladha yake, tunatamani pia tupate yale maji *fresh* pia sisi tunywe tufurahi. Kwa hivyo nimesimama kuiunga hoja hii mkono na pia ni Mwanachama wa Kamati ya Maji nawaomba pia tuiungeni mkono. Sisi kama Mwanachama wa Bunge hili, kwa sababu maji ni uhai, maji ni uzima na mwanadamu anatakikana anywe maji ambayo ni masafi. Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono. Ahsante sana.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Thank you. Yes, Honourable Makanga.

Hon. Makanga: Ahsante Mheshimiwa Spika na mimi nasimama kuunga mkono hoja hii ambayo imeletwa na Chifu Emeritus Madam Maryam Baimu ambaye kabla ya kuja kwa Bunge hili alikua ni msemaji wa serikali kuu lakini hivi sasa tunaona anafanya kinachosema Katiba ya Kenya Article (1) *that all sovereignty belongs to the people of Kenya and shall be exercised only in accordance to this Constitution*, Article (3) *the sovereign power under this Constitution is delegated to the following state organs which shall perform the functions in accordance with this Constitution*. Sub Article (4) *the sovereign power of the people is exercised at the national level and the County level*. Honourable Speaker, when you go to Schedule 4 of the Constitution of Kenya maybe if you allow me to refer to it Mr. Speaker it speaks about the functions of the County government and in it the issue of water is clearly outlined to be a function of the County government and therefore Mr. Speaker whatever the Honourable Member has done today is not only representing the people which is her duty according to the Constitution but also shows how sensitive she is to take up this matter and to speak on behalf of the people in this Honourable House. Mr. Speaker, I therefore stand to support the same that we pass this Motion and the Chair responsible for the said department not only to take action but to be proactive to make sure the Committee takes full responsibility to task the department to ensure that our people get water and not public relations management. Thank you so much Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Yes, Honourable Maryam Baimu, please reply to the Motion.

Hon. Baimu: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mimi ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waheshimiwa wenzangu wote kuweza kuunga mkono huu Mswada. Ahsante Bwana Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Honourable Members, I now stand to put a question that the Motion titled Measures to address shortage of fresh water in Mombasa County by Honourable Maryam Baimu be adopted in this House.

[Question proposed and agreed to]

Yes Clerk?

ADJOURNMENT

Honourable Members, this House stands adjourned till Wednesday 6th March, 2024 at 2:30p.m.

The House rose at 10:50a.m